**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**

S.L.P 42

**SINGIDA**

---

**Kumb. Na. IDC/B.1/8'B'/73** 18/06/2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi amepokea kibali cha Ajira mpya chenye Kumb Na. FA.97/228/01/A/25 cha tarehe 29 Aprili, 2025 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Hivyo anatangazia Watanzania wote wenye Sifa kutuma maombi kwa nafasi zifuatazo;

1.1 **MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI 2**

**1.2 SIFA ZA MWOMBAJI:**

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) aliyehitimu Stashahada (NTA level 6) katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali mwenye ujuzi wa Computa.

**1.1.2 KAZI NA MAJUKUMU**:

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masijala kwenye regista (incoming correspondence register).
ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi (outgoing correspondence register).
iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (action officers).
iv. Kupokea majalada yanayorudi masijala kutoka kwa watendaji.
v. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji.
vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (file tracking).

**1.1.3** Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali - **TGS C**.

## 1.2 DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 4

### 1.2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.2.2 MAJUKUMU NA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya Usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari “Log-Book.
vi. Kufanya usafi wa gari.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA:

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali - **TGS B**.

## 1.3 MUHUDUMU WA JIKONI (KITCHEN ATTENDANT I) DARAJA LA I - NAFASI 2

### 1.3.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu kidato cha nne mwenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

### 1.3.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kusafisha vyombo vya kupikia
ii. Kusafisha vyombo ya kulia chakula

iii. Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia chakula.
iv. Kuwatayarishia wapishi/waandazi vifaa vya mpishi na mezani
v. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
vi. Kuwasaidia Waandazi wa Wapishi

### 1.3.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara wa kuanzia ni kima cha serikali katika ngazi ya **TGOS. A**.

## 1.4 MSAIDIZI MAENDELEO YA JAMII DARAJA II - NAFASI 4

### 1.4.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe mwenye Cheti cha Kidato cha Nne (IV), Awe mwenye Astashhada (Certificate) ya Maendeleo ya Jamii kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo; Maendeleo ya Jamii (Community Development), Sayansi ya Jamii (Sociology) Mipango na Usimamizi wa Miradi (Project Planning and Management), Rural Development, Au fani nyingine zinazofanana na Maendeleo ya Jamii.

### 1.4.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kusaidia kubuni na kupanga mipango na miradi ya maendeleo katika eneo lake.
ii. Kushiriki katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.
iii. Kusaidia kutoa elimu kuhusu kazi za kujitegemea katika eneo lake.
iv. Kuandaa na kutoa taarifa za kazi za maendeleo ya Jamii kila mwezi kwa uongozi wa Kijiji na kwa Msimamizi wake wa kazi.
v. Kusaidia kuunda vikundi vya Jamii na vya maendeleo.
vi. Kutambua na kuwezesha kaya masikini kuinua uchumi wao kupitia fursa na rasilimali zinazowazunguka.

### 1.4.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara wa kuanzia ni kima cha serikali katika ngazi ya **TGS B**.

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 45 na umri usiopungua miaka 18,
- Waombaji waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika,
- Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya Taaluma na vyeti vya kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbali mbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kwenye Mfumo wa Ajira Portal
- Testimonials “Provision Results”,” Statement of Results” Hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Sita HAVITAKUBALIKA,
- Waombaji wote waweke picha mbili “Passport Size” ya hivi karibuni katika ukurasa wa Ajira Portal
- Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka husika yaani TCU, NECTA na NACTE
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
- **Waombaji kazi wa kada ya Dereva Daraja la II wenye leseni daraja E au C wanapaswa KUAMBATISHA vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.**

- Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka kwenye Kumb. Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 29 Novemba, 2010.
- Uwasilishwaji taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **01 Julai, 2025**

- **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

    Mkurugenzi Mtendaji,
    Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi
    S.L.P 42,
    **SINGIDA.**

- Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa Kielekroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia Anuani ifuatayo http://portal.ajira.go.tz, Anuani hii inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘’Recruitment portal’’.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA**:

Imetolewana;

Kastori Msigala
MKURUGENZI MTENDAJI
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**